



**COUNTY ASSEMBLY OF MOMBASA
THE HANSARD**

Tuesday, 21st November, 2023

Third Assembly – Second Session
NINETY FIFTH SITTING

*[The County Assembly met at 2:36p.m at the County Assembly Buildings]
[The Deputy Speaker (Honourable Fadhili Mwalimu Makarani) in the Chair]*

PRAYERS

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Have your seats Members. Yes, Clerk Order number one please.

MOTION

ESTABLISHMENT OF PUBLIC TOILETS FOR ENHANCED SANITATION AND ECONOMIC OPPORTUNITIES

Honourable Allen Katana, MCA Shanzu Ward.

Hon. Katana: Thank you, Honourable Speaker. I beg Mr. Speaker may I be heard in silence?

[Loud consultations]

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Members order! Proceed Honourable Allen!

Hon. Katana: Mr. Speaker, I beg to move the following Motion.

AWARE THAT access to clean and well-maintained public toilets is essential for ensuring proper sanitation, cleanliness, and public health;

FURTHER AWARE THAT the current lack of adequate public toilets in various Wards and the Central Business District (CBD) poses challenges to residents, visitors, and the overall status of the County;

UNDERSCORING the need to address the deficiencies in public toilet infrastructure to enhance the overall well-being of the community;

DISCLAIMER: The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor Page 1

NOTING THAT the establishment of public toilets in every Ward, with a special emphasis on increasing facilities in the Central Business District (CBD), would significantly contribute to improving sanitation, cleanliness, and the general public health of the Community;

RECOGNIZING THAT public toilets can serve as vital economic hubs if managed effectively, creating employment opportunities and fostering entrepreneurship among youth, women groups and other local entrepreneurs;

ASSERTING THAT leasing the management of public toilets to local community groups and entrepreneurs will not only ensure their effective maintenance but also contribute to economic empowerment and business opportunities;

CONCERNED THAT the absence of accessible public toilets hampers efforts to maintain a clean and healthy environment in the County;

SERIOUSLY CONCERNED THAT the overall image and status of the County may be adversely affected due to inadequate sanitation facilities;

I, therefore, urge this August Assembly to RESOLVE:

1. THAT the County government takes immediate action to construct and establish public toilets in every Ward, with an increased focus on enhancing facilities in the Central Business District (CBD);

2. THAT the County government explore innovative approaches, such as leasing the management of public toilets to youth groups, women groups, and other entrepreneurs, to ensure effective maintenance and create employment opportunities;

3. THAT the relevant County departments collaborate with community stakeholders to identify suitable locations for the construction of public toilets, ensuring strategic placement for maximum accessibility;

4. THAT public awareness campaigns be initiated to educate the public on the proper use and maintenance of public toilets, fostering a sense of responsibility and community ownership;

5. THAT the County government regularly monitors and evaluates the effectiveness of this initiative, making necessary adjustments to improve its impact on sanitation, cleanliness and public health.

Mr. Speaker, I therefore humbly ask the Honourable Milka to second this Motion. I thank you Mr. Speaker.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Yes, Honourable Milka?

Hon. Ngare: Thank you. Mr. Speaker, I do second the Motion.

[Applause]

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Thank you.

Honourable Members, I now propose a question that the Motion by Honourable Allen Katana on Establishment of Public Toilets for Enhanced Sanitation and Economic Opportunities be debated in this House.

[Question proposed and agreed to]

Yes, Honourable Allen Katana?

Hon. Katana: Mheshimiwa Spika nikushukuru tena kwa kunipa nafasi hii ili kutoa maelezo machache kuhusu suala hili. Mheshimiwa Spika, mimi sitakuwa mwingi wa maneno kwa sababu Waheshimiwa unao waona hapa wote wamesoma na wote ni wajanja, weledi sana wa kuelewa shida zinazo tukumba kama jiji la Mombasa. Mheshimiwa Spika niseme bila kuogopa ni kwamba Waheshimiwa wengi walio hapa Mheshimiwa walinisaidia haswa katika kujenga Hoja hii, ili kwa sababu hizi shida wanazona kila mahali na kwa sababu Waheshimiwa hawa unao waona hapa si malimbukeni wametembea kwingi na wamejionea jinsi nchi zilivyoendelea zinavyofanya shughuli zake za miji. Katika shughuli hizi mtu yeyote anaye kula ni lazima atakuwa na haja ya namna yeyote. Kwa hivyo ni muhimu ya kwamba tukaweze kuwa na sehemu hizi ambazo ni za kujisaidia ili mbali na kwamba zitakuwa zimewezesha zimerahisisha wananchi katika sehemu hizi vile vile zitakuwa zinaleta vipato katika vijana na vikundi vya wa mama ambao hawana ajira.

Mheshimiwa Spika tunaelewa miji mikubwa tukizingatia kama mji wetu mkubwa wa Nairobi nitasema sehemu nyingi utakazoenda katika mji ule zinakosa hata baadhi ya shughuli hizi. Kwa hivyo sisi kama viongozi wa jiji hili la Mombasa Mheshimiwa Spika ninaamini tutakapo pitisha suala hili mji wetu wa Mombasa utakuwa ni wa kupigiwa mfano. Mwanzo tutaimarisha mazingira yetu, pili utasaidia wageni watalii na wenyeji ambao wanaingia na kutoka katika jiji hili letu kwa sababu atakapo banwa mtu kuna mahali pa kwenda kujisaidia. Mheshimiwa Spika niruhusu niwape Waheshimiwa hawa wenye akili na hekima kubwa wapate kuchangia swala hili na kwa pamoja naamini kwa kuwa waheshimiwa Mwenyezi Mungu aliwabariki na akili, hapatakuwa na hata mmoja wa kupinga kwa sababu swala hili walinisaidia wao ili lifike katika Bunge hili. Ahsante Mheshimiwa Spika.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Yes, Honourable Benard Ogutu.

Hon. Ogutu: Ahsante sana Mheshimiwa Spika, nimesimama kuunga hoja hii...

[Applause]

Asilimia 100 Mheshimiwa Spika alivyotangulia kusema kwamba tulikaa kama Waheshimiwa ndio tukaja na hii hoja na mimi niliweza kushiriki kwa sababu kuna siku nilikutana na Mheshimiwa Allen Katana mjini akiwa anatoka jasho, Mheshimiwa nikamuuliza ni nini mbaya kwani una homa, akasema ni hali vile ambayo ana...

[Laughter]

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Proceed Honourable Ogutu.

Hon. Ogutu: Ni hali vile ambayo ana...

[Laughter]

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Okay. Thank you Honourable Ogotu. Order! Order! Honourable Madialo. Yes, Honourable Milka.

Hon. Ngare: Thank you Mr. Speaker for allowing me to give my contribution on the Motion ahead of us and I stand to support this very important Motion. Infact when I saw this Motion this morning, I kind of smiled because I was cooking something similar on sanitation because recently, I had an opportunity to attend a seminar and I presented a paper on sanitation which is really very important in society so we need such localized action to deal with sanitation issues. I know the Honourable Members and other Members have already done their research and they are aware that we have a budget for this under the department that deals with public sanitation and my happiness is that women groups will be involved as per one of the prayers of Honourable Katana and youth groups in the grassroots they will be involved in the management of such kind of infrastructure. That way they will gain an income and they will ensure that the public toilets are clean and to the standards so, that we do not have to allow the community to acquire diseases like diarrhoea, cholera and others because of poor sanitation and lack of public toilets. Something else that the Honourable Members has touched is about maintenance of the existing public toilets especially the ones in the CBD if you walk towards Mbaraki there is after the cemetery there is a public toilet there that is so poorly maintained. One time I managed to pass there I was with other Honourable Members; I cannot remember who it was and the public toilet is in dire need of maintenance you cannot imagine that a human being can get there and come out without getting an infectious disease so, we need as much as we are craving for more public toilets we also need to have the ones that are there being properly maintained and this is a chance we are losing of our youth who can properly maintain the toilets the public toilets earn a living and also ensure that it is safe for use by you, me and other people. So, I support this motion 100 per cent...

[Applause]

And the faster we pass this Motion so that we can have proper public sanitation the better for us and for the citizens of this County. Thank you, Mr. Katana, for coming up with such an important Motion which should be supported by everybody. Thank you, Mr. Speaker, for giving me the chance.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Thank you. Yes, Honourable Manuari.

Hon. Juma Manuari: Ahsante Mheshimiwa Spika kwa nafasi hii ya mchana. Mimi kubwa zaidi ni kukwambia Mheshimiwa Spika ndugu yetu Rodgers ametoa mwelekeo mzuri na saa hii nadhani sote hapa hili swala tumekubaliana nalo na kwa kuwa saa hii ni mda wa kusinzia wewe ungetanguliza tu lile swali ukatuuliza ili maana hii ishapita haina mjadala, hii imeenda. Ahsante Mheshimiwa Spika.

[Applause]

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Thank you, Yes Honourable Florence.

Hon. Kachumbo: Thank you Mr. Speaker for this opportunity...

[Interruption]

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Yes, what is it Honourable Frankline?

Hon. Makanga: Ahsante Mheshimiwa Spika.

Ilikuwa naomba Mheshimiwa Juma Manuari Mwakilishaji wa Bofu, a *withdraw statement* kwamba ni masaa ya kulala, sisi hatulali sisi wote ni wachapa kazi.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Yes, Honourable Manuari, please withdraw.

Hon. Juma Manuari: Mheshimiwa Spika yeye ameniambia ni *withdraw* lakini ni kiukweli wa maneno; hili neno kuwa ni mda wa kulala yeye ndio nimemuona akisinzia ndio maana nikasema hili neno. Kwa hivyo Mheshimiwa Spika ni yeye aseme samahani chakula kimekuwa kingi tumboni. Ahsante.

[Applause]

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Honourable Florence, please proceed?

Hon. Mwachumbo: Thank you Mr. Speaker for this opportunity to air my views. I would like to congratulate my fellow colleague Honourable Allen Katana for this thoughtful thing he is doing for the citizens. This is a very good idea and so many people out there are suffering due to lack enough public facilities like toilets for people. So, this very good idea and it will help our relatives and parents out there who usually do their things in the markets, public areas and they need this facility. So, I urge the whole House to support this. Thank you.

[Applause]

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Yes, Honourable Mbaya?

Hon. Hamisi Mbaya: Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kunipatia fursa hii baada ya kupata chakula cha mchana ambacho kinaleta usingizi pia. Mheshimiwa Spika nimesimama kuunga mkono hoja hii na pamoja ya kwamba huwa kuelewa kwangu kwa Kiingereza huwa kuko chini, lakini Mheshimiwa Spika kutokana na hoja hii ilivyotolewa Kiingereza, nimeweza kuelewa na kuweza kunifanya mimi niende moja kwa moja niweze kuunga mkono hoja hii. Ahsante sana Mheshimiwa Spika na nimeunga mkono kwa asilimia sabini, zinatoshia ahsante sana Mheshimiwa Spika.

[Laughter]
[Loud murmurings]

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Yes, the mover of the Motion please respond?

Hon. Katana: Mheshimiwa Spika nishukuru kwanza uongozi wako tena zaidi, niwashukuru Waheshimiwa wa awamu ya tatu kwa hekima waliyo nayo kubwa sana na kwa ufupi tu kama nilivyotangulia kusema ni kwamba uko mfano ndani ya Kaunti yetu ya Mombasa kuna vijana ambao mimi mwenyewe nimewapa kusimamia sehemu hizi za kujisaidia na nataka nitangaze hapa hawa vijana kwa mwezi kama ni pesa kidogo wametengeza ni shilingi laki moja na elfu hamsini (Kshs.150,000.00). Kwa hivyo Mheshimiwa Spika mbali na kwamba itakuwa imewezesha ukaaji ndani ya jiji letu kuwa rahisi kwa sababu ya hizi nafasi zitakazo kuwa mahali pa kujisaidia haja kubwa, haja ndogo na pia kuoga na kubadilisha nina hakika pia itakuwa imetengeza ajira ambalo ndio gonjwa sugu sana katika Kaunti yetu. Nimalize kwa kusema tena, kwa sababu hata Mwenyezi Mungu anasema roho isiotoa shukrani ilaaniwe Waheshimiwa wenza Mwenyezi Mungu awabariki kwa hekima yenu na tuendelee kuwatumikia wananchi wetu. Ahsante Mheshimiwa Spika.

[Applause]

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Honourable Members I now stand to put a question that the Motion by Honourable Allen Katana on *Establishment of Public Toilets for Enhanced Sanitation and Economic Opportunities* be adopted this Honourable House.

[Question put and agreed to]

[Applause]

Honourable Members, the Motion on *Establishment of Public Toilets for Enhanced Sanitation and Economic Opportunities* has been adopted by the House?

ADJOURNMENT

Members, there being no other Business the House stands adjourned until 22nd November, 2023 at 10:00 a.m.

The House rose at 2:59 p.m.